SportPesa
TZS. 1,198,475,840
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



## Mo Dewji bilionea pekee EAC ripoti mpya utajiri Afrika

UKURASA 3




# Nipashe

Jumamosi Aprili 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580931

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

### RIPOTI YA CAG

# Taasisi yafichua ulaji wa tril. 3.4/-



• Yataka serikali ichukue hatua, Zitto ahofia upigaji zaidi kuibuka... *Ukurasa. 2*





Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa aliyekuwa Rais wa Kenya, Hayati Mwai Kibaki, wakati wa Ibada ya mazishi kitaifa, katika Uwanja wa Nyayo,Nairobi, Kenya jana. Picha ndogo: Dk. Mpango akimfariji Rais wa nchi hiyo, Uhuru Kenyatta. **PICHA: OMR**

## Jela miaka 30 kunajisi mtoto wa dada yake

UKURASA 3

## Vita Russia, Ukraine vyapaisha bei ya dhahabu soko la dunia

UKURASA 2

**MICHEZO** JESHI STARS, JKT KIBARUANI UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga (wa pili kulia), akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo, wakikagua nauli kwenye mabasi ya abiria katika stendi ya mabasi ya mikoani ya Igumbilo, Manispaa ya Iringa jana, baada ya baadhi ya wasafirishaji kupandisha nauli kiholela. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Taasisi yafichua ulaji Tril. 3.4/-

**Na Sanula Athanas**

TAASISI ya WAJIBU imechambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 na kubainisha hatari ya kupotea kwa Sh. trilioni 3.365 kutokana na viashiria vya rushwa na ufisadi.

Ripoti hiyo ya CAG ilikabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan Machi 30, mwaka huu kisha kuwasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka huu na hivyo kuwa wazi kwa umma.

Katika hafla iliyoandaliwa na Policy Forum jijini Dar es Salaam, Taasisi ya WAJIBU iliyo chini ya uongozi wa Ofisa Mtendaji Mkuu, Ludovick Utouh (CAG wa zamani), iliwasilisha uchambuzi wake kuhusu ripoti hiyo ya CAG, ikimulika hoja mbalimbali zikiwamo zinazogusa haki za wananchi.

Meneja wa Utafiti na Miradi wa Taasisi ya WAJIBU, Moses Kimaro, akiwasilisha mada kuhusu viashiria vya rushwa na ufisadi, alisema jumla ya Sh. bilioni 3,365.59 (Sh. trilioni 33.365) ziko hatarini kupotea kutokana na kuwapo kwa viashiria hivyo vilivyoibuliwa na CAG Charles Kichere.

Alisema kuwa hiyo inatokana na kutozingatiwa kwa taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba; upotevu wa mapato kutokana na dosari za mifumo; miamala kufanyika mara mbili na kutofuatilia akaunti za benki.

"WAJIBU imeainisha maeneo yenye viashiria vya rushwa na ufisadi yakiwa na jumla ya Sh. bilioni 3,365.59, sawa na asilimia 13 ya bajeti nzima ya matumizi ya Sh. bilioni 25,920.36 kwa mwaka fedha 2020/21 na ongezeko kulinganishwa na Sh. bilioni 1,770.84 kwa mwaka wa fedha 2019/20," Kimaro alisema.

Meneja huyo alifafanua kuwa mchanganuo wa Sh. trilioni 33.365 zilizo hatarini kupotea kutokana na viashiria hivyo vya rushwa na ufisadi kwa mwaka 2020/21 unajumuisha: Sh. bilioni 1,993.69 (Sh. trilioni 1.994) za Serikali Kuu; Sh. bilioni 74.02 za Miradi ya Maendeleo; Sh. bilioni 122.6 za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sh. bilioni 1,175.28 (Sh. trilioni 1.175) za mashirika ya umma na taasisi za serikali.

Kimaro pia alibainisha kuwapo ukiukwaji wa haki za binadamu, akirejea Ripoti ya CAG kuhusu hali ya magereza nchini iliyoanika kwamba kati ya magereza 15 yaliyokaguliwa, manane hayakuwa na huduma ya maji safi kwa wafungwa, mahabusu na watendaji wa magereza.

Vilevile, CAG alikuta magereza yakiwa hayana huduma za matibabu na watalaamu wa afya (asilimia 78 hadi 80), kuwapo idadi kubwa ya wafungwa na mahabusu (Keko asilimia 194, Kiomboi asilimia 128) na magereza mawili tu yalikuwa na mfumo wa kamera za usalama (CCTV), utambuzi wa vifaa hatarishi (metal detectors and scanners).

Kimaro pia alirejea ripoti ya CAG kuhusu utoaji wa haki mahakamani, iliyobainisha kwamba kuna ucheleweshaji mkubwa wa upelelezi wa mashauri huku kukiwa na idadi ndogo ya mawakili wa serikali.

Katika uchambuzi wake, Taasisi ya WAJIBU pia imemulika hoja za vikwazo vya uwekezaji nchini na dosari katika utoaji na ukusanyaji wa fedha za mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu unaotekelezwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

**MAREKEBISHO YA KATIBA**

Akiwasilisha mapendekezo ya taasisi hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya WAJIBU, Yona Killagane, alisema kuna haja kufanyike marekebisho kwenye Katiba ya nchi, hasa kwenye Ibara ya 90(2-b) inayompa mamlaka Rais wa Tanzania kulivunja Bunge ikiwa wabunge watakataa kupitisha bajeti ya serikali.

Alisema kuna haja kurekebisha kifungu hicho kwa kuwa kinaweka ugumu kwa Bunge kufuatilia uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa kuwa wabunge wanakuwa na hofu ya kupoteza nafasi zao za uwakilishi pindi wakitaka kuikataa bajeti ya serikali.

Killagane pia alisema Taasisi ya WAJIBU inapendekeza serikali kuhakikisha inaboresha mazingira ya kufanya biashara nchini ili kuvutia wawekezaji, pia wananchi wadai uwajibikaji wa serikali kwao.

Mwenyekiti huyo pia alisema taasisi yao inaishauri serikali kusimamia utekelezaji wa kanuni za mwaka 2019 katika utoaji wa mikopo kwa ajili ya uwezeshaji wa makundi maalum (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya halmashauri.

"Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu ripoti hii ya CAG kwenye vyombo vya habari kwa wiki mbili sasa. Wanancghi wanajadili kuhusu usimmizi wa mapato na matumizi, lakini licha ya wananchi hao kutaka uwajibikaji, bado hakuna hatua kubwa iliyochukuliwa na serikali," alisema.

**HADHARI YA ZITTO**

Katika mjadala wa wasilisho hilo la Taasisi ya WAJIBU, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema kuna haja serikali kuchukua hatua dhidi ya waliotajwa na CAG, vinginevyo kutakuwa na 'upigaji' mkubwa katika ripoti zinazofuata.

"Mwaka 2012 kulikuwa na ripoti kama hii ambayo ilitolewa na CAG Utouh na kuibua mambo makubwa. Kuna miaka kunakuwa na hoja za kawaida kwenye ripoti lakini ripoti ya mwaka huu ni mbaya zaidi kuliko ya mwaka 2012.

"Katika kipindi changu cha uongozi wa PAC (Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali) sijawahi kuona ripoti mbaya kama hii, lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

"Utouh alitoa ripoti ambayo ilikuwa mbaya sana kwa wakati ule na mawaziri wanane walifutwa kazi. Ninafikiri jambo kubwa zaidi linapaswa kufanyika hata kama siyo mawaziri kufutwa kazi, siyo lazima iwe sawa na mwaka 2012. Vinginevyo mwakani hali itakuwa mbaya zaidi," Zitto alitahadharisha.

Zitto pia alishauri kuangaliwe upya majukumu ya CAG kwa kuwa ilivyo sasa anatekeleza zaidi jukumu la ukaguzi badala ya udhibiti, akipendekeza mabadiliko ya Katiba ya nchi yazingatie udhibiti uhamishiwe kwa wakaguzi wa ndani.

Rais wa Chama cha Wakaguzi wa Ndani Tanzania, Zelia Njeza, alisema kutowajibika kwa watendaji ndani ya taasisi za serikali, wakiwamo wakaguzi wa ndani ni ndicho kiini cha dosari zinazoibuliwa na CAG.

"Utekelezaji wa hoja ya ukaguzi uwe sehemu ya upimaji wa utendaji wa watumishi wa taasisi na hasa wakaguzi wa ndani," alishauri.

Christopher Mageka kutoka Kampuni ya Innovex Auditors, alisema kuna haja kujiuliza swali kwamba 'haya yanayoripotiwa na CAG kila mwaka ni matokeo ya kutokuwa na uwajibikaji au kutokuwa na sheria nzuri?' kisha kuchukua hatua kurekebisha lilipo tatizo.

## Vita Russia, Ukraine vyapaisha bei ya dhahabu soko la dunia

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

VITA kati ya Ukraine na Russia vimepandisha bei ya dhahabu katika soko la dunia baada ya wakia kupanda kutoka Dola za Marekani 1,412.98 (Sh. milioni 3.2) kwa Julai 2019 hadi Dola 1,947.83 (zaidi ya Sh. milioni 4.5) Machi, mwaka huu.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/23 huku akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 83.4.

Biteko alisema kuongezeka kwa bei ya dhahabu kumetokana pia na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwapo wa ugonjwa wa UVIKO-19.

"Uchumi wa madini nchini kwa kiasi kikubwa unatokana na madini ya dhahabu ambayo huchangia takribani asilimia 80 ya mapato yatokanayo na rasilimali madini. Wachambuzi wa masuala ya uchumi duniani walitarajia bei ya dhahabu kuendelea kuwa tulivu kwa mwaka 2022.

"Hata hivyo, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia imepanda kutoka wastani wa Dola za Marekani 1,412.98 Julai 2019 hadi kufikia 1,947.83 Machi, 2022. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwapo wa UVIKO-19." alisema Biteko.

Biteko alisema athari ya vita kati ya Russia na Ukraine inaweza kusababisha mahitaji makubwa ya madini ya dhahabu, akitoa sababu kwamba watu na taasisi duniani hupendelea kuhifadhi thamani ya fedha zao katika madini ya dhahabu kwa kuwa ni amana iliyo salama zaidi hasa wakati wa mitikisiko ya kiuchumi.

Waziri Biteko alisema mwaka 2021 bei ya madini ya almasi katika soko la dunia iliongezeka na kufikia wastani wa Dola za Marekani 241 kwa karati, ikilinganishwa na wastani wa Dola za Marekani 150 kwa karati mwaka 2020.

Alisema hadi Februari, mwaka huu, bei ya almasi iliendelea kuongezeka na kufikia wastani wa Dola za Marekani 369 kwa karati na kwamba ongezeko hilo limetokana na kupungua kwa mlipuko wa UVIKO-19 na uhitaji mkubwa wa bidhaa za usonara zinazotumia almasi uliojitokeza katika kipindi cha sikukuu za krismasi na mwaka mpya.Waziri Biteko alisema kuna viashiria vya bei ya almasi kwa mwaka 2022 kubadilika kwa kupanda au kushuka kutokana na Russia ambayo ni mzalishaji mkubwa wa almasi duniani kuwa katika vita na Ukraine.

"Ili kunufaika na ongezeko la bei za madini, wizara inakusudia kuchukua hatua mbalimbali, ikiwamo kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na kuangalia uwezekano wa kupunguzwa kwa baadhi ya kodi na tozo kwa wachimbaji ili kuwaongezea wigo wa faida na kuchochea uzalishaji zaidi.," alisema Biteko.

Kuhusu utoroshaji madini, Waziri Biteko alisema mojawapo ya hatua zilizochukuliwa na serikali katika kuimarisha ukusanyaji maduhuli ni pamoja na kudhibiti biashara haramu na utoroshaji wa madini.

Alisema kazi hiyo hufanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwamo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Idara ya Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, kamati za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya pamoja na raia wema. Biteko alisema katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, mwaka huu, madini ya aina mbalimbali yakiwamo dhahabu, vito, mchanga na madini ya viwandani yenye thamani ya Sh. milioni 501.2 yalikamatwa katika matukio ya utoroshaji na biashara haramu katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Manyara, Dodoma, Lindi, Geita, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza.

SOMA HOTUBA UK. 9-16

HABARI KITAIFA

# Mo Dewji bilionea pekee EAC ripoti mpya ya utajiri

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI mpya ya utajiri barani Afrika iliyotolewa na kampuni ya utafiti ya Henley & Partners, imemtaja mfanyabishara Mtanzania Mohamed Dewji, maarufu Mo Dewji kuwa bilionea pekee kutoka Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya Utajiri barani Afrika 2022, Tanzania ina wafanyabiashara 2,400 wenye utajiri wa zaidi ya Dola za Marekani milioni moja (zaidi ya Sh. bilioni 2.3).

Hata hivyo, ripoti ya hivi karibuni ya Forbes kuhusu mabilionea duniani mwaka 2022, ilibainisha kuwa Mo Dewji anaendelea kuwa mtu tajiri zaidi nchini na anachuana na mabilionea wengine wa Afrika.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya Forbes, Mo Dewji ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa MeTL Group, anashika nafasi ya 15 akiwa na utajiri unaofikia Dola za Marekani bilioni 1.5.

Ripoti mpya inabainisha makundi ya watu wenye utajiri wa kuanzia Dola za Marekani bilioni moja, wenye utajiri wa kuanzia Dola milioni 100 (centi-millionaires), wenye utajiri wa kuanzia Dola milioni 10 (multi-millionaires), wenye utajiri wa kuanzia Dola milioni moja (millionaires) na wenye utajiri wa kuanzia Dola 100,000 (mass affluent).

Inabainisha kuwa kwa kuzingatia vigezo hivyo, Tanzania ina wafanyabiashara zaidi ya 2,400 wenye utajiri wa Dola milioni moja (zaidi ya Sh. bilioni 2.3), watafiti hao wamesema idadi ya mabilionea nchini inaongezeka pale kiwango hicho kinapothaminishwa kwa Shilingi ya Tanzania.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa zaidi ya nusu ya mabilionea hao (1,300) wanaishi Dar es Salaam. inafafanuliwa zaidi kwenye ripoti hiyo kwamba Tanzania ina wafanyabiashara wanane wenye utajiri unaoanzia Dola milioni 100 (centi-millionaires) wakati Watanzania walio katika kundi la multimillionaires (utajiri wa kuanzia Dola milioni 10) ni 80.

Ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika, ripoti hiyo inabainisha kuwa Afrika Kusini ina mabilionea 39,300 ikifuatiwa na Misri (16,900) na Nigeria (10,000).

Ripoti hiyo inabainisha kuwa Tanzania ni ya saba kwa kuzingatia kigezo cha utajiri wa kuanzia Dola milioni 10 (Sh. bilioni 23b) ikiwa na matajiri 80 wa kundi hilo nyuma ya Ghana (120), Morocco (220), Kenya (340), Nigeria (510), Misri (880) na Afrika Kusini (2,080).

Tanzania imeorodheshwa kwenye nafasi ya sita kwa kigezo cha kuwa na mabilionea wenye utajiri wa Dola milioni 100 (Sh. bilioni 230).

Kuna matajiri wanane wa aina hiyo nchini nyuma ya Kenya yenye 15, Morocco (22), Nigeria (28), Misri (57) na Afrika Kusini (94).

Inafafanuliwa zaidi katika ripoti hiyo kwamba vigezo vilivyotumika ni kuzingatia takwimu za utajiri zilizopo ulimwenguni, pia takwimu za Henley & Partners zinazohusisha watu binafsi, hasa wakurugenzi, maofisa watendaji wakuu (CEO), waasisi na washirika.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Af-



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, akizungumza wakati wa kikao kazi kilichowakutanisha viongozi wa wilaya hiyo, maofisa wa Jeshi la Polisi na Wenyeviti wa Serikali za mitaa wilayani humo, mkoani Dar es Salaam jana. Mkuu huyo, aliwapa siku saba wenyeviti wa Serikali za mitaa kuhakikisha kuwa mitaa yote ambayo haina ulinzi shirikishi iwe imeanzisha. Kulia ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miaka 30 kwa kunajisi mtoto wa dada yake

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Rebucheri, Tarime mkoani Mara, Mandashi Marwa (23), amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumnajisi mtoto wa dada yake.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Yohana Myomba katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime, mjini hapa.

Marwa ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Rebucheri Halmashauri ya Mji Tarime, alidaiwa kufanya kitendo hicho dhidi ya mtoto wa dada yake ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili (majina ya mwanafunzi na shule yanahifadhiwa).

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Myombo alisema kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri, mahakama imeridhika pasina shaka lolote, hivyo kumtia hatiani mshtakiwa chini ya kifungu cha 130 (1) e na 131 cha 3 cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 mapitio ya 2019.

"Nakuhukumu kwenda jela miaka 30 ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia mbaya kama wewe, wanaoharibu maisha ya watoto wa watu wengine. Kama hukuridhika na adhabu hii, rufaa (rufani) iko wazi,"alisema Hakimu Myombo.

Kwa mujibu wa mwendesha mashtaka wa polisi, Bugombe Bukuru, mshtakiwa alimfanyia mtoto huyo kitendo hicho kwa nyakati tofauti usiku kati ya Juni na Agosti, 2021. Bukuru alidai kuwa mama wa mtoto huyo, aligundua mtoto wake kufanyiwa kitendo hicho na kuumizwa vibaya huku akishindwa kutembea.

Alidai kuwa baada ya kumbana, alimtaja mjomba wake, Marwa, hivyo kwenda kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi Tarime na kupewa fomu namba tatu (PF 3) na kumpeleka hospitalini kupimwa ma kupatiwa matibabu ambako aligundulika kunajisiwa na kuumizwa vibaya sehemu za siri.

Kutokana na taarifa hizo kufikishwa polisi, mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

Baada ya kusomewa mashtaka, mshtakiwa alikana ndipo jamhuri ilipopeleka mashahidi wanne, akiwamo daktari wa Hospitali ya Wilaya aliyemfanyia mwanafunzi huyo uchunguzi.

Mashahidi wengine waliojenga ushahidi uliomtia hatiani mshtakiwa ni mtoto aliyefanyiwa kitendo hicho, mama wa mtoto na mwalimu wa shule anayosoma mtoto huyo. Mshtakiwa alimpeleka shahidi mmoja ambaye ni mke wake, Pendo Marwa, pamoja na kujitetea mwenyewe.

# Mgogoro jiji, uongozi wa soko washika kasi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MGOGORO wa wafanyabiashara wa soko la Sabasaba na jiji la Dodoma umechukua sura mpya baada ya viongozi wa soko hilo kudai kuwa wako tayari kuuwawa badala ya kukubali kuondolewa katika eneo hilo.

Pia wamesema kutokana na viongozi wa jiji kutaka kuwaondoa bila kuwashirikisha, wanaandaa timu ya watu ambayo itakwenda kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan kumfikishia kilio chao.

Mwenyekiti wa soko hilo, Athumani Makole, alibainisha hayo jana sokoni hapo alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wafanyabiashara kujadili kuondolewa kwao katika eneo hilo.

Makole alisema hawako tayari kuondoka katika eneo hilo bila kujua hatma yao na biashara zao na wapi wanapelekwa.

"Hatutaondoka hapa tuko tayari waje watuuwe katika eneo hili wanataka kutuondoa bila kufanya mazungumzo na sisi, hivyo hatutaondoka hadi waje tukubaliane kuhusu mikopo yetu, biashara zetu na wapi wanakotupeleka.

"Kama watashindwa kukubaliana na kile tunachokihitaji, tunakwenda kumwona Rais Samia Suluhu Hassan ili atusaidie kuna watu wanamdanganya Rais kuhusu jambo hili. Sasa tutakwenda wenyewe na kama pia huko tutashindwa tutamwachia Mungu ashughulike nao," alisema.

Aidha, alisema mgogoro huo unakichafua Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na watendaji wake kuwanyanyasa wafanyabiashara ndani ya soko hilo.

"Soko hili lina wafanyabiashara 7,800 na idadi hii ni kura ambazo watendaji wa serikali wanataka kumkosesha Rais wakati wa uchaguzi mkuu mwaka 2025," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Soko, Kombo Kombo, aliwataka wafanyabiashara hao kushikamana ili kutetea haki yao ambayo uongozi wa jiji unataka kuwapokonya.

Kombo alisema kutokana kupigania haki zao, viongozi wa soko hilo maisha yao yamekuwa hatarini kutokana na kupata vitisho kutoka katika maeneo mbalimbali.

"Leo (jana) hii walikuwa wamepanga kunikamata lakini kutokana na umoja wetu wameshindwa, hivyo nawaomba ndugu zangu wafanyabiashara tuendelee kushikamana kwa umoja wetu ili kutetea maslahi yetu. Haya ndiyo maisha yetu tunatunza familia zetu hatuwezi kuondolewa tuu kama mzigo hata uhuru wa nchi hii ulipatikana kwa mazungumzo mkurugenzi aje tuzungumze anaogopa nini," alisema Kombo.

Hivi karibuni, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akizungumza na vyombo vya habari, alisema hawana lengo la kuwaondoa wafanyabiashara hao bali wanachotaka ni kuwahamisha kwa muda kupisha ujenzi wa soko hilo.

Alisema lengo la jiji ni kuwahamisha kwa muda ili kufanya ukarabati wa soko hilo na baadaye watawarejesha kuendelea na shughuli zao kama ilivyo sasa.

"Soko hili limekuwa la muda sana toka mwaka 1996 halijafanyiwa ukarabati miundominu yake ni mibovu sana ndiyo maana leo hii mvua ikinyesha tope linakuwa la kutisha na tunapokea simu za malalamiko kuwa tunachukua ushuru lakini hatufanyi ukarabati," alisema Mafuru.

Pia alisema jiji halina lengo la kuwaonea wafanyabiashara bali kinachotakiwa ni kuwashirikisha kila hatua ili kuweza kupata uelewa wa pamoja na kila mtu kuridhika na maamuzi hayo.

# Vijana 4,000 kunufaika mafunzo ya bure VETA

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA), imesema vijana 4,000 wanatarajiwa kunufaika na mafunzo mbalimbali bila ada yatakayowawezesha kujiajiri na kuanzisha viwanda vyao.

Mradi huo unaofahamika kama E4D unafadhiliwa na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Korea (KOICA) na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa kutoa pia vifaa vya kufundishia na utatekelezwa na VETA .

Akizungumza kwenye mkutano wa siku moja kuhusu utekelezaji wa mpango huo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Antony Kasore, alisema watawafundisha vijana hao masuala mbalimbali ya ufundi wa viwandani.

Kasore alisema kwenye mpango huo, watawapa mafunzo ambayo yanaendana na soko la ajira na mahitaji ya waajiri wanaotaka vijana wenye weledi na ujuzi wa kutosha kwenye maeneo mbalimbali ya kazi.

Alisema programu hiyo itafanyika kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Dodoma na Lindi na kwamba kwa asilimia 30, kozi zitatolewa katika mfumo wa kidijitali kwa kutumia simu lakini wakati wa mafunzo ya vitendo watakwenda kwenye vyuo vya VETA.

"Asilimia 70 hawa watakuwa wakiingia madarasani kupata mafunzo na tunaamini mafunzo haya yataenda kuboresha maisha ya watanzania kwa kuwawezesha vijana kupata ajira kwa urahisi na wengine kujiajiri," alisema.

Pia alisema manufaa ya mradi huo ambao ni wa mwaka mmoja na nusu yatakuwa makubwa kwa Watanzania na ulianzia Novemba, mwaka jana, na kukamilika Juni, mwakani.

Alisema vijana hao wanapatikana kupitia matangazo mbalimbali na vigezo vinawekwa kwa wanaotaka kuomba fursa hiyo ili washindanishwe na hatimaye kuwapata wale watakaoshiriki kwenye mafunzo hayo.

Kabongo Mbuyi, Kiongozi wa GIZ, alisema mradi kama huo ni wa kikanda na shirika lake limekuwa likitekeleza miradi kama hiyo kwenye nchi za Ghana, Uganda, Kenya, Afrika Kusini, Msumbiji and Nigeria.

"Mradi huu unalenga kuwapa ujuzi hasa vijana waweze kujiajiri katika nyanja mbalimbali na tunatarajia kuwekeza Dola za Marekani 4.8 na unatarajiwa kukamilika Juni 2023," alisema



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), akikabidhi tuzo ya mshindi wa pili, Sekta za Fedha kwa Mkuu wa kitengo cha Ulinzi, Usalama na Mwendelezo wa Biashara wa Benki ya CRDB, Misana Mutani baada ya benki hiyo kuibuka mshindi katika maadhimisho ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi. Tuzo hiyo pamoja na ile ya Mshindi wa Jumla wa Huduma za Jamii ya OSHA zilitolewa wakati wa ufungaji wa maonesho ya OSHA kitaifa jijini Dodoma juzi. Katikati ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Patrobas Katambi. **PICHA: CRDB**

# Muhongo ataja mambo sita kukuza uchumi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Musoma Vijijini (CCM), Prof. Sospeter Muhongo, ametaja mambo sita ambayo yatasaidia Tanzania kwenda mbele kiuchumi.

Hata hivyo, Prof. Muhongo amesema pasipo nchi kufikia asilimia nane hadi 10 ya ukuaji wa uchumi, Watanzania ni vigumu kujinasua kutoka katika umasikini.

Prof. Muhongo ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini, alitaja mambo yanayoweza kuivusha Tanzania kiuchumi kuwa ni ni kilimo, uvuvi, ufugaji, kuwa na akiba ya dhahabu Benki Kuu, uchimbaji wa gesi ya helium pamoja na madini.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Madini bungeni jana, Prof. Muhongo alisema: "Naishauri Wizara ya Madini ifanye kazi na Benki Kuu (BoT), tuanze kuwa na gold reserve (akiba ya dhahabu)."

Prof. Muhongo alisema endapo serikali itaweka akiba ya dhahabu BoT, itasaidia kuimarisha sarafu ya nchi pamoja na kusaidia mfumuko wa bei na kutokuwa na hatari ya aina yoyote. "Kwa kuthibitisha hiyo, angalia wakubwa wote duniani akiba walizo nazo. Wa kwanza ni Marekani ana akiba ya dhahabu tani 8,133, wa pili ni Ujerumani ana akiba ya dhahabu tani 3,359, wa tatu ni Italy, wa nne ni Ufaransa, wa tano ni Russia ana akiba ya dhahabu tani 2,302, wa sita ni China ana akiba ya dhahabu tani 1,948.

"Sasa hawa wakubwa wenye uchumi mkubwa na wanalinda uchumi wa nchi zao kwa kuwa na Gold Reserves kwa nini sisi Tanzania tusifanye hivyo?" alihoji Muhongo na kuongeza kuwa hata nchi zinazopakana na Tanzania zenye uchumi mdogo, zimeweka akiba ya dhahabu.

Alitolea mfano wa Msumbiji ambayo alisema ina akiba ya dhahabu tani 3.94, Burundi tani 0.03 na Kenya tani 0.02.

"Ndugu zangu uchumi usipokuwa kwa kadri ya asilimia nane hadi 10 na kuendelea hatuwezi kufuta umasikini. Sasa hivi tupo asilimia 4.8 ni lazima tufike asilimia nane. Kitu kitakachotusaidia hapo ni kwenye sekta za uwekezaji muhimu kama vile kilimo, uvuvi, ufugaji. Kingine kitakachotusaidia ni lazima twende katika uchumi wa gesi." Alisema.

Kuhusu madini, Profesa Muhongo alisema kwa miaka 20 ijayo madini yatakayohitajika duniani, Tanzania hatujaanza kuyachimba, Hivyo aliishauri Serikali kuipa uwezo Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST).

Alisema ili kufikia asilimia 10 ya uchumi ni lazima serikali ijielekeze katika kuchimba gesi ya 'helium'.

"Hii gesi haipo Wizara ya Nishati. Kwa taratibu za nchi yetu inasimamiwa na Wizara ya Madini. Sasa hivi hii gesi ipo Rukwa, huko duniani wanahitaji cubic fee bilioni sita kwa mwaka, soko lake litakuwa na thamani ya Dola za Marekani bilioni 16," alibainisha.

Alisema mtumiaji mkubwa wa gesi hiyo ni Kituo cha Anga cha Marekani cha NASA kinachotumia cubic milioni 100 kwa mwaka.

"Naomba twende kwenye uwekezaji wa gesi ya helium ili tupige hatua kiuchumi. Madini yanayohitajika duniani kwenye magari, majeshi na nishati," alisisitiza.

Alisema China imeshatangaza kwamba ifikapo mwaka 2025 inataka kuachana na magari ya mafuta wanataka madini, hivyo serikali inapaswa kujielekeza huko.

Prof. Muhongo aliyataja madini yatakayokuwa na soko miaka 20 ijayo ni pamoja na kobati, chromium, lithium, paradium, zinki, manganisi, gadium, indium pamoja na madini ya kutengeneza mbolea.

# Asakwa tuhuma za mauaji ya mkewe

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linamsaka Joshua Mlale (28) makazi wa Kitongoji cha Sisi kwa Sisi, kijiji cha Magazini wilayani Namtumbo kwa tuhuma za kumuua mke wake, Amina Chande (22) kwa kumkata na kitu tumboni huku chanzo kikidaiwa kuwa wivu wa mapenzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 25, mwaka huu, majira ya saa 4:00 asubuhi katika kitongoji cha Tuwe Macho, kijiji cha Magazini.

Konyo alisema Chande aliuawa kwa kukatwa shingoni kwa kisu na mumewe huyo na kwamba taarifa zinabainisha kuwa wawili hao walikuwa na mgogoro wa muda mrefu, hivyo wakawa hawakai nyumba moja baada ya kutengana.

Alisema kutokana na mgogoro huo, Chande alirudi nyumbani kwao ambako si mbali na anapoishi Mlale na Aprili 25 majira ya saa 4:00 asubuhi Mlale alimhadaa Chande ampe mtoto akae naye kwa muda ndipo alipewa mtoto na akaenda naye nyumbani kwake.

Alisema baadaye kidogo, Mlale alimwambia Chande aende akamchukue mtoto na alipofika nyumbani kwake kwa nia ya kumchukua, ndipo mtuhumiwa alipoamua kumkamata na kumkata shingoni kwa kutumia kisu kisha akakimbilia kusikojulikana.

Kamanda Konyo alisema juhudi za polisi za kumsaka mtuhumiwa zinaendelea na kwamba endapo atapatikana atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kumfikisha mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili.

Kuhusu mtoto, Konyo alisema yuko katika afya mzuri na anaendelea kutunzwa na mama mzazi wa marehemu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga wapeni raha mashabiki wenu

**WATANI** wa jadi, Simba na Yanga wanatarajia kukutana katika mechi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Katika mechi ya kwanza msimu huu wa 2021/2022 ambayo ilifanyika Desemba 11, mwaka jana kwenye uwanja huo huo, vigogo hao walitoka sare ya bila kufungana.

Hata hivyo, Yanga itaingia uwanjani ikiwa ndio vinara wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 16 lakini ikiwa na rekodi ya kutopoteza mchezo hata mmoja tangu kuanza kwa msimu huu, wakati Simba wao ndio mabingwa watetezi wa misimu minne mfululizo.

Wekundu wa Msimbazi pia wataikabili Yanga ikiwa bado na joto la mashindano ya kimataifa, ingawa imeondolewa kwenye hatua ya robo fainali na Orlando Pirates ya Afrika Kusini kwa penalti kufuatia matokeo ya jumla kufungana bao 1-1.

Mechi hiyo ambayo inatarajia kuendelea kutoa sura ya mbio za ubingwa, ni mchezo unaosubiriwa kwa hamu na mashabiki mbalimbali wa soka barani Afrika, na hiyo ni kutokana na ukongwe wa klabu hizo zote za Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Endapo Yanga itapata ushindi katika mchezo wa leo, itakuwa imeendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo wakati Simba itarejesha matumaini ya kulibakisha taji inalolishikilia lakini pia itasaidia kupunguza machungu ya kuondolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa heshima ya mchezo wenyewe, wachezaji wanatarajiwa kujituma na kuonyesha ubora wao katika kuhakikisha wanapata ushindi na kufikia malengo waliyojiwekea msimu huu.

Kila mchezaji anatakiwa afahamu mechi hiyo inatarajiwa kuangaliwa na wadau mbalimbali wa mpira wa miguu, hivyo kuonyesha kiwango bora na nidhamu, kutasaidia kuwatangaza na hatimaye kupata ofa zitakazoboresha maisha yao.

Hatutarajii kuona nidhamu mbaya kabla na baada ya mchezo kumalizika kwa sababu kupitia mechi hiyo, wachezaji chipukizi wanajifunza vitu mbalimbali na endapo vitendo vya hovyo vitachukua nafasi, huenda ikaharibu ukubwa wa dabi hiyo kwa nyota wanaochipukia.

Tunazo kumbukumbu kuna baadhi ya wachezaji waliopata mafanikio baada ya kumalizika kwa mechi ya dabi kutokana na ubora waliouonyesha kwa klabu zao kuwapata mikataba mipya yenye maslahi zaidi lakini pia wapo nyota 'waliopotea' baada ya kumalizika kwa mitanange hiyo ya watani wa jadi.

Soka la sasa ni la kiufundi, wachezaji na viongozi wa benchi la ufundi hakikisheni mnawaandaa wachezaji wenu kufanya yale yanayostahili katika kuhakikisha wanapata ushindi, lakini pia waheshimu waamuzi ambao wamepewa dhamana ya kusimamia mechi hiyo.

Waamuzi pia wanatakiwa kufanya kazi yao kwa umakini na weledi kwa sababu kupendelea upande mmoja kunaweza kusababisha mechi kuharibika au kuamsha hasira kwa timu iliyoonewa, kutafsiri vyema sheria 17 za soka ndio kutasaidia kila timu kuvuna ilichokipanda.

Ikumbukwe waamuzi wanaposhindwa kumudu mchezo, hupunguza pia raha ya aliyeshinda kushangilia ushindi wake.

Bila kusahau mashabiki watakaojitokeza uwanjani kushuhudia mchezo huo wanatakiwa wafahamu mipaka na nafasi yao. Kila shabiki anatakiwa ahakikishe anashangilia kwa nidhamu na bila kuharibu miundombinu iliyowekwa kwenye uwanja huo unaomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kutumia maneno makali kwa wachezaji, waamuzi au mashabiki wenyewe kwa wenyewe ni mambo yasitotakiwa kuonekana kwenye mchezo huo ambao huvutia wadau wa soka kutoka mataifa ya jirani.

Simba na Yanga, mbali na kusaka pointi, tumieni mechi hiyo kwa kuipa heshima na hadhi inayostahili Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imeweza kupanda viwango na kushika nafasi za juu barani Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachambuzi, wasemaji wajiepushe na upotoshaji

**DUNIA** ya sasa ya soka kumekuwa na watu wanaoitwa wachambuzi ambao kwa kiasi kikubwa wameufanya mchezo huo kuendelea kupendwa na mashabiki mbalimbali.

Wala siyo siri kabla ya wachambuzi hakukuwa na idadi kubwa ya mashabiki kama hivi sasa, lakini wachambuzi kutokana na kulizungumzia soka kwa ufasaha na ufafanuzi wa kina, limeonekana kupiga hatua kwa kupendwa na wengi.

Sipendi sana watu wanaowasakama wachambuzi kwa sababu watu hao ndiyo wameleta utamu wa mchezo huo, ingawa ni kweli baadhi yao wameonekana ni tatizo.

Tatizo la mtu mmoja mmoja, haliwezi kuwafanya wachambuzi wote waonekane wabaya.

Ni kwamba Maofisa Habari na wasemaji , ingawa hao wanaonekana hawaonyeshewi vidole baadhi yao hawatofautiani na baadhi ya wachambuzi. Kuna wakati wanakiuka na kwenda mbali zaidi ya kazi yao ya usemaji.

Wapo wasemaji badala ya kuzisemea timu zao, wao kutwa kazi yao kuelezea ubaya wa timu nyingine.

Sisemi kama kusiwe na utani, upo, lakini kwa asilimia ndogo. Msemaji kwa kiasi kikubwa anatakiwa kuiongelea na kuisifia timu yake kama vile anavyofanya Masau Bwire, hata kama haipo katika kiwango au ubora anaoizungumzia. Na asilimia chache zilizobaki utaitania timu ambayo unacheza nayo, huu ndiyo mpira kwa sababu kutaniana kupo na hata kupigana vijembe.

Sijaona Masau au Thobias Kifaru wakienda kwenye vyombo vya habari kuizungumzia timu nyingine kwa muda mwingi, kuliko kile kilichompeleka kuizungumzia timu yake.

Wakati mwingine inakuwa si utani tena, bali ni kuidhalilisha, kuitupia lawama taasisi nyingine na kuituhumu vitu ambavyo kama si kujificha kwenye kivuli cha soka, basi ni kesi kubwa inayoweza kumpeleka mtu mahakamani.

Pia kwa siku za karibuni kumezuka na mtindo wa wasemaji kuanza kuwasema watu binafsi, mambo binafsi badala ya klabu au timu.

Unashangaa kwenye redio, watu hawataniani tena mpira, badala yake mambo binafsi, na kutuhumiana uchawi na mambo yasiyofaa inashangaza.

Hapo ndipo nalia na watangazaji na wachambuzi, kumwacha mtu akituhumu mambo ya uchawi, kitu ambacho kwa kawaida hakina ushahidi na si vizuri kumwacha mtu kuelezea kitu ambacho kisheria iwapo mtuhumiwa akitaka ushahidi huwezi kuupata.

Najua inafanywa kwa kisingizio cha utani, lakini kwenye chombo cha habari ni hatari kwa sababu inaaminisha watu wengine kuamini mambo ya kishirikina, si kwenye soka tu, hata kwenye mambo mengine ya maisha, watapatikana watu ambao kila anachotaka kukifanya, au kinachompata, basi anaamini ni uchawi tu.

Vipindi vya michezo vya asubuhi kwa sasa vinafuatiliwa na watu wengi na vinapendwa, hivyo visiruhusu sana wasemaji wanaokuja kupotosha kwa makusudi au kwa bahati mbaya kwa sababu, mashabiki wengi wanawaamini sana wachambuzi na wasemaji hao, hivyo kulishwa uongo ambao nao wanakuwa wanausambaza.

Inashangaza kuona msemaji anasema timu yake msimu ujao itaanza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika moja kwa moja katika raundi ya kwanza na si ya awali, huku wachambuzi wakimwacha tu akipotosha.

Sijajua kama na wao walikuwa hawajui au la. Ni hivi, ili timu icheze raundi ya kwanza ni lazima iwe angalau kwenye zile 20 bora za juu. Ni klabu 10 tu za juu ndizo zinazotakiwa kuanza raundi ya kwanza, zilizobaki zote zinaanzia awali. Sasa inawezekana kuanzia ya 11 hadi ya 20 ikacheza kama zile 10 za juu hazitokuwa bingwa kwenye nchi zao. Mfano timu inayoshika nafasi ya 10 kama si bingwa au ya pili kutegemea nchi hiyo inaingiza timu ngapi, basi ya 11 inachukua nafasi. Kama ya nane, tisa na 10 hazikuwa bingwa nchini mwao, basi ya 11, 12 na 13 zinachukua nafasi hizo kama watakuwa mabingwa, ili mradi zile 10.

Sasa unashangaa timu inashika nafasi ya 50, 60 hadi 70, leo unaambiwa haitocheza awali. Labda timu 40 hadi 50 zote za juu zisiwe mabingwa nchini mwao, kitu ambacho hakiwezekani.

Mtu aongea kwenye redio na wachambuzi wako kimya. Mbali na kuchambua mechi husika, wachambuzi pia wanatakiwa kusoma vitu vingi tofauti vya soka, ili kukabiliana na aina hii ya upotoshaji. Siku hizi vitu vyote viko kwenye mtandao, wala haitumii nguvu kuvipata, nibando lako tu. Fanyeni hivi ili kuusaidia mpira wa Tanzania kuendelea na si kila siku kuendeleza mipasho, na upotoshaji usio na kichwa wala miguu, ambao pia unaweza kuvishushia heshima vyombo hivyo, watangazaji na wachambuzi wenyewe.

MAKALA

# Nyimbo za mchakamchaka shuleni enzi hizo

## ■Makaburu, Amin, Banda, Kambona walikiona

Na Adam Fungamwango



SIKU hizi nadhani kwenye shule nyingi hakuna mchakamchaka. Na kama upo, basi ni ule tu wa kawaida sana ambao watoto hawakimbii umbali mrefu. Labda kuzunguka shule tu, wasije watoto wa watu wakaanguka ikawa balaa. Watoto wa siku hizi bwana. Kwa sasa ukiona mchakamchaka barabarani basi ni kikundi cha 'joging'. Kusema kweli watoto wa zamani walikuwa wakakamavu sana kuliko wa sasa. Hawa wa sasa ni werevu mno, yaani wanajua vitu mapema tofauti na umri wao tofauti na wa zamani, lakini linapokuja kwenye suala la ukakamavu, wa zamani walikuwa fiti.

Shule zote Tanzania zilikuwa na kipindi cha kukimbia mchakamchaka asubuhi. Zingine mara moja kwa wiki. Kuna mara mbili na hata mara tatu. Mara tatu mara nyingi inakuwa Ijumaa.

Huu ndiyo mchakamchaka mkubwa zaidi au tuseme ndiyo wanafunzi wanakimbia umbali mrefu sana kutoka shuleni na kuzunguka huko na huko kabla ya kurejea tena. Kwa nini kulikuwa na mchakamchaka?

Uliwafundisha wanafunzi uzalendo, kuwa wakakamavu, kupendana, kujaliana, umoja, na kujiona kama ndugu, kusaidiana na mengine mengi, hasa kipindi kile cha maisha ya ujamaa.

Uliwafanya pia kuwa werevu darasani, kujiamini, ukichochea ukuaji wa uwezo wa akili kwa mwanafunzi, misuli na mapafu.

Ulisababisha kugundua baadhi ya vipaji vilivyojificha kwa wanafunzi kama vile kuimba, au kukimbia.

Na hata wanafunzi wenye matatizo ya kiafya waligundulika kwenye mchakamchaka na kuanza kutibiwa mapema kabla ugonjwa kuwa sugu.

Kwa wakati huo wanafunzi wengi walipenda sana kipindi cha mchakamchaka kwa sababu kilionekana na kufanana kama kipindi cha michezo hivi, watu wakikimbia na kuimba.

Sasa twende kwenye nyimbo zenyewe. Mara nyingi nyimbo ziligawanyika sehemu mbili.

Nyimbo za hamasa, uzalendo wa nchi, kusifia viongozi wa Tanzania na hata wa nje lakini wenye mlengo wa siasa za nchi hii, kuwaponda mabeberu wa Afrika Kusini ambao wakati huo nchi nyingi za Kusini mwa Afrika kama Namibia, Angola, Zimbabwe, Zambia na Afrika kusini bado hazikuwa huru. Baadaye moja baada ya nyingine ikaanza kuwa huru, lakini haikupunguza nyimbo za kimapinduzi ambapo zilianza kutoweka kwenye miaka ya 1990, hasa baada ya Afrika Kusini kuwa nchini ya mwisho kupata Uhuru.

Ni wakati huo kukawa na nyimbo nyingi za kuwasema, kuwazodoa makaburu wa kusini mwa Afrika.

Mwaka 1978, wakati Nduli Idd Amin wa Uganda aliivamia Tanzania, naye pamoja na kuchapwa, lakini pia alitungiwa nyimbo za kumshushua, kumtisha na kumkejeli, hadi Tanzania iliposhinda vita.

Wakati Mwalimu Nyerere alipoamua kutangaza Azimio la Arusha mwaka 1967, mmoja wa waziri aliyehitilafiana naye ni Oscar Kambona. Yeye hakupenda mlengo wa Ujamaa na Kujitegemea, hivyo akatimkia nchini Uingereza. Basi zilitungwa nyimbo za mchakamchaka zilizoimbwa mashuleni na 'zilimnanga' kweli.

Kamuzu Banda yeye alikuwa Rais wa Malawi wakati huo. Huyu mara kwa mara alikuwa akiichokonoa Tanzania, akidai sehemu ya ardhi ya Tanzania na Ziwa Nyasa ni mali ya Malawi. Na yeye aliipatapata kwenye nyimbo za hamasa. Kama nyimbo za kunanga watu zingekuwa zinaua, basi Kambona, Banda na Amin wangekufa wakati ule ule.

Upande wa pili kukawa na nyimbo za kumsifu Hayati Mwalimu Nyerere. Hizi nazo zilikuwa nyingi sana.

"Iddi Amin akifa, mimi siwezi kulia. Nitamtupa Kagera, awe chakula cha mamba."" Watanzania tumevamiwa na joka kubwa. Idd Amin, acheni tuliponde sasa, limezoea, tumeshachoka, sasa tuliue joka..."

"Lile lile lilembe, mbaya sana Amin, kafikiria sana kashindwa, kaona akachue Kagera, ambayo ni ardhi ya Tanzania."

"Idd Amin Jasusi ambalo ni joka kuu, limefanya uvamizi kuteka ardhi yetu, hakuna jambo lingine ni kumfunza adabu, ndipo litakapojua Tanzania ni ya watu." Ni ya nyimbo aliyoimbiwa Amin kwenye mchakamchaka.

"Alisema alisema, alisema Nyerere alisema, vijana wangu wote mmelegea. Sasa tuanze mchakamchaka chinja." "Nani ajuaye Nyerere kabambe? Sisi tunajua Nyerere ni mwenyewe. Aje simba mtu, aje simba mtu." Ni kati ya baadhi ya nyimbo nyingi za kumsifu Nyerere kwa kazi kubwa aliyoifanyia nchi hii.

"Kaburu matata hiya hiya...vijana mmechoka? Bado. Mbona hamuimbi? Tunaimba. Kimbunga cha nini? Chahamia mpakani." Huu ni moja kati ya nyimbo za kizalendo na kimapinduzi zilizokuwa zikipinga ubaguzi wa watu weusi, Afrika Kusini.

"Banda aa aa Banda, ana wazimu, Kambona kawekwa Ulaya. Na nani? Na Mabeberu."

"Banda wa Malawi katuvamia ngozi ya Simba kutitisha Watanzania, hatujali ooo..."

Hizo ni nyimbo maarufu zilizokuwa zikiimbwa kwenye mchachakamchaka kwenye shule ya msingi na sekondari, hata kwenye halaiki.

Ikumbukwe nyimbo hizi pia zilikuwa zikiimbwa hata kwenye mafunzo ya Mgambo, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Na inavyoonekana ni kwamba zilianzia huko na walimu walizichukua na kuziingiza mashuleni.

Zilikuwepo nyingi sana na zingine ni za kawaida tu, wala si za Makaburu, Kambona wala Amin.

Hata wanafunzi wenyewe walikuwa na uwezo wa kujitungia nyimbo zao na kuziimba kutokana na mazingira ya sehemu husika, mfano Dar es Salaam, mwanzoni mwa miaka ya 1980, Dar es Salaam kulikuwa na daladala moja maarufu likiitwa Simba Luwala, lilitungiwa wimbo.

Lakini hizi ziliimbwa na wanafunzi wenyewe, wanapokimbia mchakamchaka peke yao bila walimu mbali na shule.

"Daladala Simba Luwala, chini zenge, juu makaratasi." Mikoani nako walikuwa na nyimbo zao.

"Zaina Zaina mtoto wa Ngaza, unanichanganya, nipe raha Zaina."

"Kanyaga twende, limbwata limbwata. Ng'ombe wangu ana mguu wa bia." Halafu kuna ule wa "Mama mende, mama panya." Huu ulitokana na tangazo moja maarufu redioni miaka ya katikati ya 1980, wanafunzi Tanzania nzima wakaufanya wa kukimbilia mchakamchaka.

Wanapokaribia eneo la shule wanaachana nazo na kurejea kwenye nyimbo za kawaida, zilizozoeleka za Makaburu na kina Amin.

**Tuma meseji 0716 350534**

# TPBRC YATANGAZA KUMFUNGIA BONDIA ALIYETOROKA MUHIMBILI

**Na Saada Akida**

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), imemfungia bondia, Hassan Kube miezi minne kushiriki mchezo huo kutokana na kitendo chake cha kukwepa matibabu na kutoroka katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambapo alipelekwa kwa ajili ya kutibiwa.

Uamuzi huo umetolewa na Kamati ya Afya ya TPBRC baada ya bondia huyo kukwepa matatibu kufuatia kichapo cha KO alichopigwa katika pambano la fainali ya Championi wa Kitaa lililofanyika hivi karibuni.

Kube alipigwa KO na Max Kube na kupelekea kukimbizwa katika Hospitali ya Rufaa Temeke kabla ya baadaye kuhamishiwa Muhimbili, lakini bondia huyo inaelezwa aliamua kuondoka kwa madai afya yake imeimarika.

Taarifa zilizoandikwa katika mtandao wa Boxrec, zinaonyesha bondia huyo aliyecheza mapambano sita na amepoteza matatu kwa KO, sasa hataweza kupanda ulingoni hadi Juni 18, mwaka huu adhabu yake itakapomalizika.

Gazeti hili lilimtafuta daktari, Hadija Hamisi ambaye alisimamia fainali ya Championi wa Kitaa, amekiri kumfungia bondia huyo kwa sababu ameshindwa kufuata taratibu za matatibu kama alivyotakiwa.

"Ni kweli Kube tumemfungia kucheza ngumi hadi atakapotuletea majibu ya vipimo ambavyo alitakiwa kufanyiwa, kwa sababu yeye alipelekwa katika hospitali ya Temeke ambapo walimwandikia rufaa kwenda Muhimbili lakini matokeo yake aliamua kutoroka," alisema na kuongeza.

"Zuio la Kube kutokupanda ulingoni litaendelea kuwepo ikiwa yeye hatoleta majibu ya vipimo vyake, siku ile alianguka vibaya sana na kupelekea tumpe huduma kubwa kabla ya kumkimbiza Temeke na baadaye Muhimbili," daktari huyo alisema.

**Aliongeza adhabu ambayo amepewa Kube ipo kwa mu jibu wa kanuni na taratibu za mchezo huo.**

"Hatutaki kumweka bondia kwenye hatari, hatutaruhusu bondia ambaye ameupia kupanda ulingoni bila ya kuthibitisha afya yake, hii itasaidia kulinda usalama wao pamoja na maendeleo ya mchezo wa ngumi," Hadija aliongeza.




Baadhi ya washindi wa Betika Mtoko wa Kibingwa kutoka Mtwara wakiwa wamewasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam ili kushuhudia mechi ya dabi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. Mashabiki hao wamegharamiwa na Kampuni ya michezo ya kubashiri ya Betika.**PICHA: MTANDAO**

# *Washindi Betika Mtoko watua Dar*

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI katika promosheni ya Betika Mtoko wa Kibingwa iliyotoa fursa kwa mashabiki 24 wa Simba na Yanga kushuhudia mchezo wa dabi, wamewasili jijini Dar es Salaam jana tayari kuungana na mashabiki wengine kushuhudia mchezo huo utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mara baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa jijini wakitokea mikoa mbalimbali nchini, washindi hao ambao ni wanazi wa timu hizo walitambiana wakiweka kete kwa Yanga na wengine wakiipa nafasi Simba kuondoka na pointi tatu.

Meneja Masoko wa Kampuni ya Betika, Nelson Mwanuzi, alisema washindi wote wamewasili na leo watakuwa miongoni mwa mashabiki watakaoshuhudia dabi hiyo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, Tanzania Bara kwa udhamini wa kampuni hiyo.

"Wote wamegharamiwa na Betika, watashuhudia mechi hiyo kwa hadhi ya VIP, kuanzia wakiwa hoteli hadi uwanjani na wataondoka Jumapili," alisema Mwanuzi.

Baadhi ya washindi waliishukuru kampuni ya Betika kwa kuwapa fursa ya kushuhudia mechi hiyo ya dabi huku baadhi yao wakifichua kuwa ni mara yao ya kwanza kwenda Dar es Salaam kushuhudia dabi hiyo laivu.

Sharafi Sharkati wa Mtwara alisema Betika imempa fursa ya kuja kushuhudia dabi hiyo ambayo mbali na kuwa mechi ya heshima, matokeo mazuri ni muhimu kwa timu zote mbili.

Baadhi ya washindi ni Mbaraka Selemani wa Mtwara, Justine Bulaya (Arusha), Sifa Kaminyoge (Mbeya), Lameck Ndimugangwe, Edward Zakayo (Kigoma), Peter Martin (Singida), Leopord Thobias na Masatu John wa Mwanza.

# Mabondia chipukizi kutafutwa mikoani

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI promota wa ngumi za kulipwa nchini, Selemani Semunyu akiwashukuru wadau wa mchezo huo kwa ushirikiano anaopata, ameahidi kuandaa mapambano mbalimbali mikoani kwa ajili ya kuukuza mchezo huo.

Semunyu alitoa kauli hiyo juzi katika hafla ya futari aliyoandaa maalumu kwa mabondia, makocha na viongozi wa taasisi mbalimbali zinazoshughulika na mchezo wa ngumi.

"Sina budi kuwashukuru wadau mbalimbali wa mchezo wa ngumi kwa jinsi wanavyoniunga mkono ninapoandaa mashindano, sitachoka kuuendeleza mchezo huu wa ngumi za kulipwa," alisema Semunyu.

Promota huyo alisema alifurahi kuona mwaka jana alifanikiwa kutoa zawadi ya gari kwa bingwa, ambapo ilikwenda kwa Twaha Kiduku aliyemchapa Abdallah Pazi maarufu Dulla Mbabe.

"Kwa mwaka jana pambano kubwa lilikuwa ni lile la Twaha Kiduku na Dulla Mbabe, mwaka huu litakuwa la Selemani Kidunda dhidi ya bondia kutoka Kongo, ninaamini pia wapenzi watashuhudia pambano lenye ubora," Semunyu alisema.

Kidunda na bondia huyo kutoka DRC watapanda ulingoni Julai 30, mwaka huu mkoani Ruvuma.

# Pawasa asaka kikosi cha BAFCON

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya ufukweni, Boniface Pawasa, amesema anatumia ligi ya mchezo huo inayoendelea jijini Dar es Salaam ili kupata kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Afrika.

Pawasa alisema kupitia ligi hiyo inayoshirikisha timu 13, atapata wachezaji watakaounda kikosi kitakachopeperusha bendera ya nchi.

"Ligi ya ufukweni inayochezwa katika makundi mawili ni sehemu muhimu kwangu kuangalia vipaji, inanisaidia kuongeza wachezaji wapya ambao wataitumia nchi," alisema Pawasa.

Aliongeza anahitaji kuona Tanzania inafanya vizuri zaidi katika michuano ya Afrika mwaka huu na kuendelea kuiletea nchi heshima.

"Tupo kwenye mchakato wa kuchagua timu itakayokwenda kuchuana katika mashindano ya BAFCON ambayo yatakafanyika Oktoba, mwaka huu nchini Msumbiji," alisema Pawasa.

Kocha huyo alisema wanatarajia kuingia kambini mapema kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa kufuzu utakaochezwa Julai, mwaka huu huku akitamba Tanzania iko kwenye nafasi ya saba barani Afrika katika mchezo huo.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMTAKA RASHFORD

ARSENAL inamtaka mshambuliaji wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24. (***Football Insider***)

### ROONEY ATAJWA BURNLEY

KOCHA wa Derby, Wayne Rooney anasakwa na Burnley' kama chaguo lao namba moja katika mchakato wa kumrithi Sean Dyche. (***Sun***)

### UNITED YAMWANIA ISIMHEN

KLABU ya Manchester United imeipa ishara Napoli kwamba iko tayari kulipa pauni milioni 84 kwa ajili mshambuliaji, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23. (***La Repubblica***)

### TCHOUAMENI SOKONI

LIVERPOOL inatarajia kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Monaco, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22. (***Mail***)

### TEN HAG AMTAJA DYBALA

KOCHA ajaye wa Manchester United, Erik ten Hag anataka kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28. (C***orriere dello Sport***)

### SERGIO SOKONI HISPANIA

KLABU ya Tottenham Hotspur itasikiliza ofa kwa ajili ya mlinzi wake wa kushoto, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 25, kufuatia tetesi za kutakiwa na klabu moja ya Hispania. (***Football Insider***)

### WAN-BISSAKA AGEUKA LULU

KLABU ya Crystal Palace inamtaka kwa mkopo mlinzi wa Manchester United, Aaron Wan-Bissaka. Nyota huyo mwenye umri wa miaka miaka 24 ametokea kwenye kituo cha kukuza vipaji cha Palace na ameichezea Palace michezo 42. (***Athletic***)

### TUANZEBE MAMBO MAGUMU

NAPOLI imeachana na mpango wake wa kumsajili moja kwa moja mlinzi wa Manchester United, Axel Tuanzebe. Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 24 anacheza kwa mkopo katika klabu hiyo ya Serie A tangu Januari lakini amecheza mchezo mmoja tu. (***Calciomercato, via Sun***)

### NEVES KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United imekaribishwa kuwasilisha ofa kwa ajili ya kiungo wa Wolves, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25. (***Manchester Evening News***)

### JAMES ANUKIA WEST

WEST Ham na Aston Villa ni miongoni mwa timu zinazowania kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 30 kutoka klabu ya Qatari, Al Rayyan. (***Fichajes***)

### NELSSON ATAJWA VILLA

MLINZI wa kati wa Galatasaray na Timu ya Taifa ya Denmark, Victor Nelsson mwenye umri wa miaka 23, amekuwa akihusishwa kuhamia Aston Villa. (***Tum Spor***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POCHETTINO ATANGAZA KUBAKIA NA MBAPPE

## Lakini atahadharisha lolote linaweza kutokea kuhusiana na...

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino anadai yeye na Kylian Mbappe watakuwa na "asilimia 100" Paris Saint-Germain msimu ujao.

Bosi wa PSG na mshambuliaji nyota, Mbappe wote wamedaiwa wataondoka katika mji mkuu wa Ufaransa mwishoni mwa msimu huu, huku Mbappe akihusishwa mara kwa mara na kuhamia Real Madrid wakati mkataba wake ukikaribia kuisha.

Akizungumza katika mkutano na wanahabari kabla ya mchezo wa jana dhidi ya Strasbourg, ambao ni wa kwanza tangu washinde taji la Ligue 1, Pochettino alionekana kuashiria mustakabali wake na wa nyota wa kimataifa wa Ufaransa kubaki katika klabu hiyo.

**Mbappe amekuwa mchezaji anayeongoza PSG msimu huu, akiwa amefunga mabao 33 na kutoa asisti 18 katika michezo 42 aliyocheza katika michuano yote.**

Alipoulizwa ni asilimia ngapi angetoa ambayo yeye na Mbappe bado watakuwa PSG mwaka ujao, Pochettino alisema: "Asilimia mia moja, katika hali zote mbili."

Akijibu swali lililofuata kuhusu kama amefanya mazungumzo na uongozi wa klabu, kocha huyo raia wa Argentina alifafanua: "Hakujakuwa na mazungumzo yoyote madhubuti, zaidi ya ilivyo kawaida katika mipango yetu na kile ambacho tumekuwa tukifanya.

"Tunaendelea kufanya kazi kwa bidii, sio tu kwa kuzingatia sasa, lakini pia na jukumu la kufikiria juu ya siku zijazo, kwa hivyo ndivyo tunafanya."

Alipotakiwa kueleza zaidi uhakika wake kuhusu Mbappe, Pochettino alisema: "Hivyo ndivyo ninavyojisikia leo. Ndivyo naweza kukuambia leo. Siwezi kusema chochote zaidi. Ndivyo ninavyojisikia kwa sasa.

"Hii ni soka, na hatujui nini kinaweza kutokea."

Licha ya kunyakua taji hilo wiki iliyopita, michezo ya hivi majuzi imeshuhudia wachezaji wengine nyota, haswa Neymar na Lionel Messi, wakizomewa na mashabiki wa PSG, na hawakuwa katika kiwango bora zaidi msimu huu.

3,475,840

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/04/22 | 17:00 | Watford vs Burnley | 2.51 | 3.20 | 2.71 |
| 02. 30/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Brighton | 2.64 | 3.04 | 2.69 |
| 03. 30/04/22 | 17:00 | Southampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.26 | 2.97 |
| 04. 30/04/22 | 14:30 | Barnsley vs Preston | 2.77 | 3.27 | 2.42 |
| 05. 30/04/22 | 17:00 | Coventry vs Huddersfield | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 06. 30/04/22 | 19:00 | Sampdoria vs Genoa | 2.46 | 3.18 | 2.79 |
| 07. 30/04/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 08. 01/05/22 | 15:00 | Elche vs Osasuna | 2.99 | 3.09 | 2.42 |
| 09. 01/05/22 | 15:30 | GO Ahead Eagles vs Vitesse Arnhem | 2.59 | 3.43 | 2.49 |
| 10. 01/05/22 | 16:00 | Empoli vs Torino | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 01/05/22 | 17:15 | Granada vs Celta Vigo | 2.56 | 3.16 | 2.76 |
| 12. 01/05/22 | 19:30 | Rayo Vallecano vs Real Sociedad | 2.96 | 3.06 | 2.47 |
| 13. 01/05/22 | 21:00 | Waalwick vs Groningen | 2.68 | 3.33 | 2.46 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 30/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1737 | Newcastle vs Liverpool | 6.73 | 4.65 | 1.40 |
| 16:00 | 1007 | Kasimpasa vs Basaksehir | 2.73 | 3.32 | 2.46 |
| 16:00 | 1056 | Cagliari vs Verona | 2.44 | 3.31 | 2.72 |
| 16:00 | 1671 | Napoli vs Sassuolo | 1.44 | 4.87 | 5.56 |
| 16:00 | 4481 | Konyaspor vs Fatih Karagumruk | 1.75 | 3.72 | 4.27 |
| 16:30 | 2236 | Borussia Dortmund vs VfL Bochum | 1.34 | 5.18 | 6.97 |
| 16:30 | 2877 | Augsburg vs FC Koln | 2.73 | 3.32 | 2.43 |
| 16:30 | 3009 | FC Krasnodar vs Rostov | 2.87 | 3.31 | 2.33 |
| 16:30 | 3922 | Arminia Bielefeld vs Hertha BSC | 2.58 | 3.13 | 2.68 |
| 16:30 | 4573 | Mainz vs Bayern Munchen | 4.98 | 4.68 | 1.50 |
| 16:30 | 4828 | Stuttgart vs VfL Wolfsburg | 2.00 | 3.47 | 3.42 |
| 17:00 | 1258 | Middlesbrough vs Stoke City | 1.80 | 3.51 | 4.16 |
| 17:00 | 1335 | Blackburn vs Bournemouth | 2.83 | 3.23 | 2.40 |
| 17:00 | 1387 | Coventry vs Huddersfield | 2.38 | 3.22 | 2.87 |
| 17:00 | 1429 | Southampton vs Crystal Palace | 2.32 | 3.27 | 2.92 |
| 17:00 | 1761 | Aston Villa vs Norwich City | 1.36 | 4.77 | 7.35 |
| 17:00 | 2103 | Cardiff vs Birmingham | 2.04 | 3.32 | 3.47 |
| 17:00 | 2561 | Millwall vs Peterborough | 1.47 | 4.18 | 6.17 |
| 17:00 | 2888 | Reading vs West Bromwich | 2.78 | 3.33 | 2.38 |
| 17:00 | 2893 | FC Arouca vs Portimonense | 1.99 | 3.32 | 3.67 |
| 17:00 | 2993 | Bristol City vs Hull City | 2.16 | 3.37 | 3.12 |
| 17:00 | 3312 | Watford vs Burnley | 2.59 | 3.18 | 2.64 |
| 17:00 | 4133 | Nottingham vs Swansea | 1.52 | 4.05 | 5.72 |
| 17:00 | 4207 | Young Africans vs Simba | 2.43 | 2.80 | 3.35 |
| 17:00 | 5074 | Blackpool vs Derby | 1.89 | 3.37 | 3.92 |
| 17:00 | 5830 | Wolverhampton vs Brighton | 2.64 | 2.98 | 2.74 |
| 17:15 | 4358 | Reggina vs Como | 2.16 | 3.26 | 3.21 |
| 17:15 | 4944 | Real Madrid vs Espanyol | 1.54 | 4.16 | 5.50 |
| 18:00 | 4918 | Lens vs Nantes | 1.62 | 3.88 | 4.98 |
| 19:00 | 4495 | Sampdoria vs Genoa | 2.63 | 3.07 | 2.68 |
| 19:00 | 5553 | Maritimo vs Benfica | 5.76 | 4.27 | 1.50 |
| 19:15 | 2765 | Eibar vs Zaragoza | 1.87 | 3.28 | 4.17 |
| 19:30 | 1309 | Zenit St Petersburg vs Lokomotiv Moscow | 1.25 | 5.73 | 9.28 |
| 19:30 | 1944 | Valencia vs Levante | 2.26 | 3.40 | 3.00 |
| 19:30 | 2532 | Leeds vs Manchester City | 7.64 | 5.10 | 1.33 |
| 19:30 | 4122 | Hoffenheim vs SC Freiburg | 2.36 | 3.47 | 2.72 |
| 19:45 | 2862 | Ajax vs PEC Zwolle | 1.10 | 8.52 | 18.82 |
| 20:00 | 4330 | Sochaux vs Bastia | 1.74 | 3.33 | 4.87 |
| 20:00 | 4507 | Niort vs Dijon | 2.40 | 3.12 | 2.92 |
| 20:00 | 4597 | Paris FC vs Valenciennes | 1.69 | 3.41 | 5.14 |
| 20:00 | 5250 | Guingamp vs Caen | 2.34 | 3.07 | 3.07 |
| 20:30 | 5054 | Trabzonspor vs Antalyaspor | 1.79 | 3.59 | 4.19 |
| 20:30 | 5135 | Hatayspor vs Altay | 1.80 | 3.64 | 4.09 |
| 21:30 | 4448 | Burgos vs Almeria | 3.66 | 3.17 | 2.04 |
| 21:30 | 5461 | SV Darmstadt vs Erzgebirge Aue | 1.33 | 5.32 | 7.10 |
| 21:45 | 2153 | RFC Seraing vs Racing White Daring Molenbeek | 2.14 | 3.13 | 3.48 |
| 21:45 | 2637 | Spezia vs Lazio | 4.74 | 3.90 | 1.63 |
| 22:00 | 2728 | Sparta Rotterdam vs AZ Alkmaar | 4.56 | 3.52 | 1.73 |
| 22:00 | 2929 | Rennes vs St Etienne | 1.30 | 5.38 | 8.17 |
| 22:00 | 3846 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.96 | 3.01 | 2.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# BASEBALL AFRIKA YAPANGWA KUFANYIKA TANZANIA MEI

**Na Saada Akida**

TANZAANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya Baseball na Softball Afrika yatakayofanyika kuanzia Mei 23 hadi 26, mwaka huu jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Mashindano hayo ni kwa ajili ya kusaka timu zitakazokata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Julai, mwaka huu nchini Mexico.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Baseball Tanzania (TABSA ), Alpherio Nchimbi alisema maandalizi kuelekea mashindano hayo yanaendelea vizuri na wamejipanga kuandaa kwa ubora wa kimataifa.

**Nchimbi alisema wameandaa mazingira mazuri kwa ajili ya timu zitakazokuja nchini kushiriki michuano hiyo itakayoshirikisha wachezaji kutoka nchi 10.**

"Tunafuraha kusema kila kitu kinaenda vizuri baada ya serikali yetu kupitia wizara husika kutuhakikishia timu hiyo itapata mahitaji yote, hivyo tutaingia katika mashindano tukiwa washindani na si wasindikizaji," Nchimbi aliongeza.

Alisema Tanzania inawakilishwa na wachezaji 12 mchanganyiko ikiwemo wavulana na wasichana kila kitu kinaenda vizuri baada ya Serikali kupitia Wizara husika kuhakikisha timu hiyo inapata mahitaji yote.

Alitayaja mataifa mengine yanayotarajiwa kushiriki mashindano hayo ni pamoja na Ghana, Kenya, Uganda, Misri, Afrika Kusini, Zambia, Zimbambwe, Tunisia na Burkinafaso.




Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakijifua kwa ajili ya kuwakaribisha Burundi katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia (U-17) itakayofanyika kesho kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar. **PICHA: TFF**

# Jeshi Stars, JKT kibaruani

**Na Saada Akida**

TIMU ya Jeshi Stars inatarajia kuvaana na JKT katika mechi ya Ligi ya Wavu Mkoa wa Dar es Salaam kwa wanawake itakayofanyika leo kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Uhuru Wasichana jijini Dar es Salaam.

Mchezo mwingine wa ligi hiyo kwa upande wa wanaume utakuwa ni kati ya Twalipo dhidi ya JKT huku Kigamboni wakitarajia kuumana na Nyika.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wavu Mkoa wa Dar es Salaam (DAREVA),Yusuph Mkalambati aliliambia gazeti hili ligi hiyo inaendelea vizuri na ushindani unazidi kuongezeka.

Mkalambati alisema ukiangalia katika msimamo kuna timu zinaongoza na baadaye nyingine zinazishusha kutokana na ushindani huo.

" Kwa kweli ligi yetu imekuwa ikitupa matumaini na inatupa nafasi ya kuibua vipaji, msimu huu timu zimesajili kikamilifu," alisema Mkalambati.

Katika msimamo wa ligi hiyo kwa upande wa wanaume, Jeshi Stars inaongoza ikiwa na pointi 14 sawa na Tanesco ambao wanashika nafasi ya pili wakati kwa wanawake Magereza yenye pointi 15 ndio vinara wakifuatiwa na Jeshi Stars yenye pointi 13.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Aprili 30, 2022



Liverpool wanogewa na Klopp

UKURASA 22



Kocha Mkuu Simba - Pablo Franco



Kocha Msaidizi Yanga - Cedrick Kaze

# Tutawafurahisha

## Ni ahadi kuelekea dabi ambayo viungo wanatarajiwa kuamua...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

SIKU iliyokuwa inasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka nchini kwa ajili ya mechi ya watani wa jadi, Yanga na Simba imefika ambapo vigogo hao watakutana katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Katika mechi ya kwanza msimu huu, timu hizo zinazofundishwa na makocha wa kigeni, zilitoka suluhu.

Akizungumzia mechi ya leo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema wanaweka takwimu pembeni na wataingia uwanjani kwa nidhamu kubwa kwa ajili ya kupambana kutafuta pointi tatu dhidi ya mpinzani wao Simba.

Kaze alisema wamejiandaa vizuri kwa sababu wanahitaji kuvuna pointi tatu kutoka kwa watani zao.

Alisema wanaenda kukutana na timu iliyokuwa bora kuanzia mchezaji mmoja mmoja hali ambayo wanalazimika kucheza kwa nidhamu na kuachana na dhana ya wao hawawezi kupoteza.

"Tunaenda kukutana na timu bora ambayo imeondolewa katika hatua ya robo fainali Afrika. Mchezo utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kutokana na wapinzani wetu wana wachezaji wazuri, lakini tutaenda kucheza kwa kuzuia na kushambulia wanapokuwa na mpira," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema katika mchezo huo watawakosa wachezaji wawili akiwamo Yacouba Sogne na Chiko Ushindi aliyeumia juzi huku Saido Ntibanzokiza akirejea na kuwa tayari kushiriki mchezo huo.

"Tunaingia katika mechi yetu kutafuta pointi tatu ili kujiweka katika mazingira mazuri kuelekea malengo yetu, ila hatuingii tukisema sisi ni bora kwa sababu hatujapoteza mechi msimu huu," alisema na aliongeza.

**"Presha inakuwa kubwa sana katika mchezo huu kutokana na nafasi za hizi timu, Yanga haijawahi kucheza dabi ikiwa nafasi ya kwanza, na tofauti kubwa ya pointi dhidi ya Simba walioko nafasi ya pili katika msimamo," alisema Kaze.**

Aliongeza wanaingia katika dabi bila kufuata historia kwa sababu misimu iliyopita timu inayoonekana bora ndio hufungwa huku akitamba mchezo huu ni tofauti.

Deus Kaseke, akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake alisema maandalizi yako salama na kila mmoja wao anahamu ya kupambana katika mchezo huo ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

"Tumejiandaa vizuri, tunawaheshimu Simba kwa sababu huu ni mchezo wa dabi ni muhimu na sasa tunaenda kupambana kutafuta pointi muhimu," alisema Kaseke.

Naye Kocha wa Simba, Pablo Franco alisema hii ni mechi kubwa na wao wamezoea kupambana na timu kubwa kama walivyotoka hivi karibuni kucheza dhidi ya Orlando Pirates.

Pablo alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu kila mmoja wao anahitaji kupata pointi muhimu na wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri.

"Tumejiandaa vizuri baada ya kutoka Afrika Kusini dhidi ya Orlando Pirates, tunawaheshimu Yanga na wachezaji wangu wako tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo bila kuangalia matokeo yaliyopita," alisema Pablo.

Alisema amefanikiwa kuyaona madhaifu na ubora wa wapinzani wao kwa kuangalia kila sehemu ikiwamo safu ya ushambuliaji na kujipanga kutopoteza mchezo huo.

Shomari Kapombe alisema wamejiandaa vizuri kwenda kuonyesha soka nzuri na kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo mazuri.

"Tumejiandaa vizuri na yoyote atakayepata nafasi atajitoa kwa asilimia kubwa, tumejipanga kwenda kuwafurahisha mashabiki wetu kwa kuondoka na pointi tatu," alisema Kapombe.

Aliongeza baada ya kupoteza dhidi ya Orlando Pirates, walikaa na kujiuliza na kuona wanahitaji kuwafurahisha mashabiki wao kwa kupata pointi tatu katika pambano hilo.

"Hatuna presha kabisa dhidi ya mchezo huu, tunaenda kupambana na kuonyesha kile ambacho mwalimu alichotupa uwanjani, na kuhusu ubingwa nina imani tunaenda kupambana katika michezo iliyobakia," alisema Kapombe.

**MECHI HAITABIRIKI- DEWJI**

Naye mfadhili wa zamani wa Simba, Azim Dewji amesema mechi za watani wa jadi siku zote huwa hazitabiriki, huku akiitakia kila la kheri timu yake kuibuka na ushindi katika mechi hiyo itakayochezeshwa na mwamuzi, Ramadhani Kayoko kutoka jijini.

"Simba na Yanga mechi zake huwezi kuzitabiri, anayetakiwa kushinda utakuta anafungwa na anayetakiwa kufungwa ndio anashinda, ina maana timu inaweza kuonekana haiko kwenye ubora msimu huo lakini ikaishinda yenye ubora, hiyo ndio 'dabi', lakini kwenye mechi hii Simba iko vizuri na inatakiwa ishinde," alisema Rage.

Hata hivyo Katibu Mkuu huyo wa zamani wa Chama cha Soka Tanzania (FAT sasa TFF), alimsifia Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi kuwa ndiye kwa kiasi kikubwa ameibadilisha timu hiyo na kuonekana hivyo ilivyo.

"Yanga nayo ni timu nzuri na ina kocha mzuri sana, ameisuka timu imekuwa bora na kwa muda mrefu Wanayanga wanakiri kuona tofauti kubwa ya uchezaji kutoka kwenye soka lao la kubutuabutua na hivi sasa wanatandaza soka kwa pasi za chini chini siyo kama zamani. Ila nawaombea ushindi Simba ili wawafurahishe wapenzi wao na wawape zawadi ya Idd," alisema Dewji.

Yanga ambayo ndiyo mwenyeji inashuka dimbani ikiwa imeizidi Simba pointi 13. kwani imefikisha pointi 54, watani zao wakiwa na pointi 41, lakini wana mchezo mmoja nyuma.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >